

**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 1**  
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**  
**SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Monday 10 May 2004 (afternoon)

Lundi 10 mai 2004 (après-midi)

Lunes 10 de mayo de 2004 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d’y être autorisé.
- Rédiger un commentaire sur un seul des passages.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento.

*Kifafanue kimoja kati ya vifungu vifwatavyo:*

1. (a)

Sauti nisikiao                      si ngeni ninaijuwa  
Si ngeni kwenye sikio              vyema ninaielewa  
Huyo awika jogoo                  na mnadi anadia  
Ujilio wa mawiyo!

5

Na rangi niionayo                  machoni yanielea  
Anga rangi lilonayo                linanitiya tamaa  
Kwamba sasa ni mawiyo          punde jua ‘tazagaa  
Hilo jua lachomoza!

10

Ona jua lachomoza                miale yake latoa  
Siku mpya ishaanza                maisha yaendelea  
Jana ishapitiliza                    na leo ishaingia  
Tusome ishara hizi!

15

Ingawa pana ukungu                angani ulozagaa  
Walakini ndugu zangu              asubuhi ishangia  
Na lile neno la Mungu              ndiyo hivi latimia  
Kwamba hubadili mambo!

20

Haya wima twamkeni!              mawiyo yashatujia  
Tusikae vitandani                  ombwe likatulemea  
Sote mbele natwendeni              mwiko nyuma kurejea  
Siku mpya ndio hii!

Kutoka *Mawiyo*, Mswada wa Mohamed Ghassany, 2003

1. (b)

Alipita karibu na mti fulani. Mti mkubwa huu. Mkuyu mnene na mrefu. Sehemu hii iliogopwa na watu wengi. Kichomi cha woga na hofu kilimkata moyoni. Alisikia sauti fulani ya kualikaalika akatamani kutoa usiahi. Lakini alijitahidi. Alitembea kinyatunyatu; kwa ncha za miguu yake. Labda alihofu kuitafiri mizimu iliyo katika madhabihu ile.

5 Alipinda sehemu fulani. Alitupa macho yake mbele. Alimwona mtu fulani ila ilikuwa vigumu kumtambua. Alihofu. Aligwaya. Alijaribu kuyakaza macho yake. Alimtambua kwa kiasi fulani; alikuwa mwanamume. Alishusha pumzi. Alimwalia; alielekea kuifuata njia hiyo aliyoifwata yeye. Yaelekea hatima yao ilikuwa moja. Mm ... Labda nia zao zilikuwa hizohizo.

10 Nzisa alishika mtandio aliokuwa amejitupia mabegani. Aliishika ncha yake begani uzuri. Aliendelea kutembea. Giza lilishatoweka sasa; aliweza kuona mbele kwa uwazi. Sehemu za juu milimani zilikuwa zimegubikwa na kiwingu cheupe; kiwingu kilichotandikiza kama shuka.

Jua lililokuwa linakucha lilianza kukonyezana na miti iliyositawi katika mlima wa 15 Kititu. Aliukaza mwendo wake. Yule mwanamme aliyekuwa mbele yake aliendelea kutembea. Hakuwa na habari kama aliandamwa nyuma. Yaelekea hakutaka kugeuka nyuma; utadhani ana maagizo kama mgonjwa wa matumbwitumbwi au anahofu kugeuka jiwe.

Alianza kupanda mlima wa Kititu. Alitupa macho nyuma upande wa kijiji cha 20 Misombe. Watu walikwisha anza kuamkaamka. Aliona viwingu viwingu vya vumbi katika viwanja vya wake wenzake ambao walishaanza kufagiafagia. Jogoo walisikika wakiwika hapa na pale; mmoja angewika hapo kisha mwengine angejibu huko. Wengine watadikia mbali huko na kuyafanya yaishie majibizano.

Aliendelea kuupanda ule mlima. Yule mwanamme alikuwa mbele bado. Alitembea 25 kwa hatua ndefu. Aliacha njia kuu kisha akapinda kushoto na kutumia njia fulani nyembamba. Sasa Nzisa alielewa; walielekea mahali palepale.

Kutoka *Nguvu ya Sala* na K.W. Wamitila, 1999